# Kristo 1





# KRISTO 1

MWANDISHI: BEN AVERY

PENSELI: SERGIO CARIELLO

INKS: SERGIO CARIELLO

RANGI: ZACH MATHENY

BARUA: TABITHA RANI

MTAFSIRI: MARCI ONSINYO

MHARIRI: REUBEN ONSINYO

KUBUNI: LISA MCMAHON

MCHAPISHAJI: KINGSTONE COMICS

---

Kimechapishwa na Comic Bible Society
Hakimiliki @2021

Kingstone Comics inahifadhi hakimiliki ya kitabu hiki ilivyoruhusiwa na sheria ya hakimiliki za Marekani.

Nakala za kuchapichwa na za dijitali za toleo hili la Kiswahili zaweza kusambazwa bure bila adhabu chini ya leseni ya Creative Commons.


KRISTO
ENEO LA YUDEA, NJE YA YERUSALEMU, KWENYE NJIA YA KUELEKEA BETLEHEMU.
KWA AJILI YA SENSA ILIYOAMRISHWA NA MAAFISA WA KIRUMI, WATU WOTE YUDEA LAZIMA WAREJEE NYUMBANI KWA MABABU.
KATI YA WASAFIRI HAO NI MARIA NA MUMEO YOSEFU.
WANAELEKEA BETLEHEMU, MAILI THEMANINI KUSINI MWA KWAO NYUMBANI NAZARETI.
MARIA, TUSIMAME. DAKIKA MOJA TU.
NIKO SAWA, YOSEFU.
TWATAKA TUFIKE KWA MDA MZURI.
KAWAIDA SAFARI INGECHUKUA SIKU NNE AU TANO TU LAKINI MARIA NI MJA MZITO.
BETLEHEMU HAIENDI KOKOTE. BADO ITAKUWEPO TUKIFIKA.
NDIO, NA HAWA WATU WOTE PIA WATAKUWEPO TUKIFIKA!
USITIE SHAKA. NINA JAMAA HUKO.
TUTAKAA KWENYE NYUMBA YA WAGENI MPAKA TUWAPATE. KILA KITU KITAKUA SAWA.
ALIVYOFANYA MARA NYINGI MIEZI MICHACHE ILIYOPITA, MARIA AJIPATA AKIWAZA KUHUSU KILICHOMFIKISHA HAPA.
NAJUA YOSEFU. NAJUA.
LUKA 2:1-4


KWENYE UJANA WAKE KAMA MWANAMKE KWENYE KIJIJI KIDOGO CHA NAZARETI ALITARAJIA MAISHA MATULIVU YENYE ITIKADI ZA KITAMADUNI.
YEYE NA MUMEWE YOSEFU WALIKUA WAMECHUMBIANA KUMAANISHA WALIKUA WAMEFUNGANISHWA PAMOJA KWENYE MKATABA WA NDOA.
LAKINI BADO WALIISHI KANDO KANDO NA JAMII ZAO.
KUFATIA UTAMADUNI WOTE WALINGOJEA USIKU AMBAO BABAKE YOSEFU ANGEMTUMA KUMCHUKUA MARIA.
KISHA KUNGEKUA NA SHEREHE YA PILI KUBWA ZAIDI.
NA YOSEFU ANGEENDA NYUMBANI NA MARIA NDIPO AKAWE BI HARUSI
MARIA! NILIMUONA YOSEFU AKIJENGA NYUMBA YENU MPYA JANA.
WAZAZI WAKO WALIKUA NA HEKIMA KUKUOZA KWA SEREMALA
KWELI!
NI MUME MZURI!
MAISHA YAO PAMOJA YANGEANZA.
MARIA ALIJUA KUWA YOSEFU, MWENYE BIDII NA MCHA MUNGU, ANGEKUA BWANA NA BABA MZURI.
WALIPANGA KUISHI KWENYE NYUMBA YOSEFU ALIYOIJENGA KARIBU NA NYUMBA YA FAMILIA YAKE NAZARETI, WAIJAZE NA WATOTO, NA WAWE PAMOJA UZEENI.
LAKINI HIYO ILIKUA MIPANGO YA VIJANA WAWILI NA MIPANGO HIYO ILIKARIBIA KUBADILIKA PAKUBWA.
SALAMU, MARIA...


WATAKA... WATAKA NINI...
HAUNA LA KUOGOPA MARIA.
KWELI MUNGU AMEPENDEZEWA NAWE.
HIVI KARIBUNI UTAPATA MIMBA NA UTAZAA MTOTO WA KIUME.
NA UTAMPA JINA LAKE YESU.


MIMI?
NDIO.
WEWE.
ATAITWA MWANA WA ALIYE JUU!
BABA MUNGU ATAMPA KITI CHA ENZI CHA MFALME DAUDI, ULIYETOKA KWENYE KIZAZI CHAKE, NA ATATAWALA JUU YA NYUMBA YA YAKOBO DAIMA.
LAKINI...
HILI LITAFANYIKAJE? YOSEFU NA MIMI BADO... HATUJA...
MIMI BADO NI BIKRA.
MARIA, MTAKATIFU UTAKAYEMZAA ATAKUA MWANA WA MUNGU!
NA HAKUNA JAMBO ASILOLIWEZA MUNGU.
HATA ELIZABETI, BINAMU YAKO, ALIVYO MZEE NA TASA TANGU UJANANI, NI MJA MZITO!
MI...
MIMI NI MTUMISHI WA BWANA,


LUKA 1:32-37


MAISHA YA MARIA SIO PEKEE YALIYO KATIZWA NA HABARI YA MALAIKA.
JOSEFU! NAHITAJI KUONGEA NAWE.
MARIA!
ANGALIA! NIMEJUA TUTAJENGA WAPI TUTAKAPOPATA WATOTO.
NA NAHITAJI KUJUA ULILITAKA JIKO WAPI!
KUNA NINI MARIA?
USITIE SHAKA, NITAPATAYARISHA MAHALI HAPA PAWE TAYARI KWA HARUSI YETU.
YOSEFU, SINA SHAKA KUHUSU HAYO... NINA JAMBO MUHIMU LA KUKWAMBIA.
NA YOSEFU AKAMSIKIZA AKAMWELEZA KILA KITU.
...NA NIMEMBEBA MTOTO HIVI SASA YOSEFU.
UNATARAJIA NIAMINI HAYA?
NIMETUMIA MDA MWINGI NA NGUVU NIKIWAJENGEA NYUMBA HII WEWE NA WATOTO WETU.
ONDOKA HAPA MARIA.
TAFADHALI.


BAADAYE MARIA ALIKWENDA KWA BINAMUYE ELIZABETI HUKO YUDEA, KIJIJI CHA MILIMANI NJE YA NAZARETI.
ASANTE KWA KUTEMBEA NAMI ZAKARIA.
MWANAWE ELIZABETI... HUTANIJIBU, SIO?
MARIA, BINAMU YANGU MPENDWA!
HUJAMBO ELIZABETI?
ELIZABETI, KUNA KITU KINACHOMTATIZA ZAKARIA? HAKUSEMA NENO LOLOTE --
OOOH!
ELIZABETI! NI MTOTO?
NDIO! NDIO! LAKINI SIVYO UNAVYODHANI!
NA ELIZABETI AKAJAWA NA ROHO MTAKATIFU.
MARIA, UMEBARIKIWA KULIKO WANAWAKE WOTE.
NA MTOTO ALIYE TUMBONI MWAKO AMEBARIKIWA!
LAKINI MIMI PIA NIMEBARIKIWA! MAANAKE NYUMBANI MWANGU AMESIMAMA BINAMU YANGU, MAMAKE MUNGU WANGU!
AH, ELIZABETI! ULIJUA... ULIJUAJE?
MARIA, MANENO YAKO YALIPONIFIKIA MASIKIONI TU, MTOTO ALIYE TUMBONI ALIRUKA KWA FURAHA!
TUNA MENGI YA KUZUMGUMZA...
LUKA 1:39-45


...KWA HIYO, NILIFURAHIA SANA ULIPONIULIZA NIJE HAPA ELIZABETI.
YOSEFU ANGETOA AMRI NIULIWE KWA KUPIGWA MAWE.
LAKINI ANAFIKIRIA TALAKA KWA KIMYA NDIO BORA: HATAKI KUOA MSHERATI, KISHA NAWEZA KUZAA MTOTO NIKAISHI NA FAMILIA YANGU.
NI MUME MZURI MARIA. MPE MDA.
ULIULIZA KAMA ZAKARIA ALIKUA SAWA. ULIJUA KUWA PIA YEYE ALITEMBELEWA NA MALAIKA?
ZAKARIA NA MIMI HATUJAWAHI KUPATA WATOTO LAKINI SIO KWA SABABU HATUKUTAKA.
TULIJARIBU. TULIOMBA. TULIKATA TAMAA.
HAIKUWA BAHATI YETU MAISHANI, TULIMWAMINI MUNGU KUWA KULIKUWA NA KUSUDIO.
LAKINI ZAKARIA ALIKUA YERUSALEMU KWA WAJIBU WAKE ILIVYOKUWA DESTURI KAMA KUHANI, ALICHAGULIWA KWA KUPIGIWA KURA KWENDA MADHABAHUNI PATAKATIFU KUENDELEA KUFUKIZA UVUMBA.
MAKUHANI HUINGIA MADHABAHUNI PEKE YAO, LAKINI GHAFLA ZAKARIA WANGU ALIJIPATA ANA MWENZAKE!
HAMNA LA KUOGOPA ZAKARIA.
MAOMBI YAKO YAMEJIBIWA. WEWE NA MKEO ELIZABETI KARIBUNI MTAPATA MTOTO MVULANA.
UTAMPA JINA YOHANA NA ATALETA FURAHA NYUMBANI MWENU.
WATU WENGI SANA WATASHANGILIA KUZALIWA KWAKE!
LUKA 1:5-14



ATAREJESHA WATU KWA BWANA MUNGU WAO, NA ATATANGULIA NA NGUVU NA ROHO YA ELIYA!
ATAWAREJESHA WAASI KWENYE HAKI!
ATAWAANDA WATU, AKITAYARISHA NJIA YA BWANA KUJA!
KWA HIYO, MUME WANGU KUHANI, MUME WANGU MWALIMU, ASEMA KWA HUYU MJUMBE KUTOKA KWA MUNGU:
ITAKUWAJE HIVI? MIMI NA MKE WANGU TU WAZEE!
MIMI NI GABRIELI! NINASIMAMA MBELE ZA MUNGU ALIYENITUMA NISEME NAWE NA NIKWAMBIE HAYA!
SASA, UTAKUWA BUBU HADI YOTE YATIMIE MAANAKE HUKUNIAMINI!
ILINICHUKUA MDA KUELEWA HADITHI MAANAK E ANAWEZA KUWASILIANA KWA ISHARA ZA MIKONO NA KUANDIKA TU.
LAKINI ALICHOKISEMA MALAIKA KIMETIMIA: ZAKARIA HAZUNGUMZI NA KUNA MTOTO ANAYEKUA TUMBONI MWANGU.
ZAKARIA WANGU, AMEPATA SOMO.
YOSEFU WAKO? YEYE PIA.
NATUMAI LAKINI NAJUA ANAVYONIFIKIRIA...
MUNGU HATAMFICHA UKWELI NA UKWELI UKIFICHULIWA YOSEFU WAKO ATATAKA KUMTUMIKIA MUNGU UNAVYOFANYA WEWE.
NINA... NINATUMAINI.
MARIA ALIKAA NA ELIZABETI KAMA MDA WA MIEZI MITATU.
HATIMAYE, ELIZABETI ALIZAAMVULANA. MAJIRANI NA JAMAA, WAKIJUA MUNGU ALIMWONYESHA WINGI WA REHEMA, WALISHEREHEKEA NAYE.
SIKU YA NANE BAADA YA KIJANA KUZALIWA ALIPELEKWA KUTAHIRIWA.
NILIKUA NATUMAINI ZAKARIA ATAKUA ANAONGEA SASA.
NILITAKA ANISIMULIE ALIVYOKUTANA NA MALAIKA.
NILITUMAI TU ANGEZUNGUMZA WAKATI WA KUTAHIRIWA.
LUKA 1:16-20


--- NA NADHANIA MTOTO ATAITWA ZAKARIA KAMA BABAKE.
LA!
YOHANA! JINA LAKE LITAKUA YOHANA!
LAKINI HAKUNA YOHANA KWA FAMILIA HII NINAYEMJUA!
KUNA YOHANA KWENU?
HAPANA LAKINI LAZIMA AITWE YOHANA!
HAIFAI UMPE JINA ZURI LA FAMILIA?
SIDHANI NINAMJUA YEYOTE ALIYE NA JINA HILO!
ZAKARIA, UNA WAZO GANI KUHUSU JAMBO HILI?
TAFADHALI MTU AKAMTWALIE ZAKARIA PA KUANDIKIA!
JINA LAKE NI YOHANA.
SAWA BASI, LITAKUWA YOHANA!
AH! BWANA ASIFIWE!!!
BWANA ASIFIWE MAANAKE AMEWAOKOA WATU WAKE!
NA WEWE MWANANGU UTAKUA NABII WA MUNGU, KUWATAYARISHA WATU KWA UKOMBOZI NA MSAMAHA WA BWANA!
NA KILA MTU ENEO HILO ALIJAWA NA MSHANGAO NA KUONGEA KUHUSU YOTE YALIYOWAFANYIKIA ZAKARIA NA ELIZABETI.






MATAYO 1:19-20




MATAYO 1:20-25


BAADAYE NYUMBANI MWA ZAKARIA NA ELIZABETI.
EH, JAMANI, UNAKAMATA KWELI!
MUNGU ALIFANYA UAMUZI SAWA KUKUULIZA UMLEE MWANAWE, U MZURI NA WATOTO.
YOSEFU, WAFANYA NINI HAPA?
MALAIKA. ALINITEMBELEA MIMI PIA.
WANIAMINI?
NDIO MARIA. BILA SHAKA.
WAONA, NILIKWAMBIA ATAELEWA.
NI MWANAMUME MZURI.
NAJUA.
NAHITAJI KUFIKA NYUMBANI --
-- KUIMALIZA NYUMBA YETU --
--LAKINI NILITAKA UJUE KILICHOTENDEKA.
KILA KITU KITAENDELEA TULIVYOPANGA KAMA BADO WATAKA.
NDIO YOSEFU, BILA SHAKA!
NIMEAHIDI KUMSAIDIA ELIZABETI NA MTOTO KWA WIKI CHACHE ZENGINE, MPAKA MAMBO YATULIE.
NJOO NYUMBANI HIVI KARIBUNI.
HATUJUI NI LINI BABANGU ATANITUMA NIKUCHUKUE LAKINI NATAKA NIWE NA UWEZO WA KUKUPATA ATAKAPOFANYA HIVYO.
MARIA ALIPORUDI NYUMBANI KUTOKA KWA BINAMUYE NA BAADA YA YOSEFU KUMALIZA KUJENGA NYUMBA YAO, WAKATI ULIFIKA BABAKE YOSEFU ALIPOMTUMA KUMCHUKUA BI HARUSI.
KWA SHANGWE, YOSEFU NA RAFIKI ZAKE WALIMLETA MARIA NJE YA NYUMBA YAO NA HARUSI IKATIMIA.
LAKINI YOSEFU HAKUJAMIIANA NAYE. ANGENGOJEA MPAKA MTOTO ALIYEAHIDIWA AZALIWE.
INGAWA MTOTO HUYO HAKUZALIWA KWENYE NYUMBA ALIYOIJENGA YOSEFU -


-- KWA SABABU MUDA MFUPI BAADA YA HARUSI, SENSA ILIAMRISHWA, AMRI YA KUWA WATU WOTE WAJISAJILI NYUMBANI KWAO KWA ASILI.
NA KWA MARA NYENGINE MARIA NA YOSEFU WALIJIPATA KWENYE MKONDO AMBAYO HAWAKUTARAJIA.
LAKINI WOTE WALIIWEKA IMANI YAO NDANI YA MUNGU WAKIJUA KUWA NI NJIA YAKE WALIYOIFUATA.
YOSEFU, NAWEZA KUTEMBEA KWA MUDA ZAIDI KIDOGO.
LABDA WAWEZ A LAKINI KWA NINI UFANYE HIVYO ILHALI SIO LAZIMA?
TWENDE.
VYUMBA VYOTE VIZURI VITACHUKULIWA.
GEUKA! RUDI NYUMBANI!
KWA NINI MNAWATII WATU WALIOCHUKUA NCHI YETU KWA KUSHIRIKI KWENYE SENSA HII?
ROMA HAINA MADAI YOYOTE KWETU SISI. MFALME ANAJIITA MUNGU LAKINI SISI TWAMTUMIKIA MUNGU MMOJA TU!
MTU ANAFAA KUMPASHA HAYO YULE ANAYEJIITA MFALME WETU, HERODE!
TUKO KARIBU KUFIKA! BETLEHEMU! KWA MABABU ZANGU! ALIKOZALIWA MFALME DAUDI!
NA ATAKOZALIWA MTOTO HUYU PIA. TWAHITAJI KUPATA MAHALI PA KUKAA YOSEFU.
NA UPESI.
TUTAKUA NA KITANDA CHENYE JOTO LEO USIKU NA TUUNGANE NA JAMAA WANGU KESHO.
NA WALIFURAHIA KUFATA NJIA HIYO PAMOJA.
LUKA 2:1-5


YERUSALEMU.
MFALME HERODE!
WEWE NI MJUMBE WA JENERALI KIRENIO, SIO?
KARIBU! NAWEZA KUKUTUMIKIA VIPI?
GAVANA KIRENIO ATAKA KUJUA SENSA INAVYOENDELEA, MFALME HERODE.
JENERALI KIRENIO NI GAVANA WA SIRIA LAKINI --
USIKOSEE MFALME HERODE, JENERALI KIRENIO AWEZA KUWA GAVANA WA YUDEA LAKINI --
-- LAKINI NDIYE ANAYEKUTAWALA WEWE.
PIGA RIPOTI KWA JENERALI KIRENIO KUWA HAKUNA LILILOBADILIKA TANGU ATUME MJUMBE KUNIANGALIA.
WATU WANAENDA VIJIJINI MWAO KAMA ROMA ILIVYOTAKA LAKINI KUNA UASI HAPA NA PALE.
AMRI YAKE IMEMALIZA UHUSIANO NILIO NAO NA WATU HAWA.
HMMMM...
SENSA INA KUSUDIO LAKE.
INAONYESHA WALIO NA UAMINIFU NA WASIO WAAMINIFU KWA ROMA NA NADHANI,KWAKO WEWE PIA.
UASI UNAOZUNGUMZIA UTATUPA FURSA YA KUPIMA UASI DHIDI YA ROMA KUTOKA KWA ENEO LAKO UTAKUAJE.
ULIPUUZA KURIPOTI YA KUWA INAONEKANA WAFARISAYO KATIKA ENEO LAKO HAWANA MPANGO YA KUHUSIKA NA SENSA.



LUKA 2:1-2



SENSA HAIJAISHA.
WAEZA KUMWAMBIA JENERALI KIRENIO KUWA YOTE YANAENDA SAWA.
NA WAEZA KUMWAMBIA KUWA HAITAJI KUTUMA VIJAKAZI WAKE KUNICHUNGUZA.
NJOO.
USHASKIA UTANI ANAOUSEMA KAISARI KUHUSU HUYU MFALME HERODE?
BWANA?
"AFADHALI NIWE NGURUWE KWENYE NYUMBA YA HERODE KULIKO MMOJA WA WATOTO WAKE," KAISARO ASEMA
HERODE AJIDAI MYAHUDI HALI NGURUWE AKITUMAINI WATU WATAMPENDA YEYE.
LAKINI AMEWALISHA JAMAA WAKE KWA MAMBA KWA SABABU ALIOGOPA WATATISHIA KITI CHAKE CHA ENZI.
ANGENITUPA KWENYE MAMBA KAMA SINGELIKUWA AFISA WA ROMA.
YULE NI MWANAMUME ALIYE TAYARI KUFANYA LOLOTE ABAKI AKITAWALA --
--LOLOTE.


BETLEHEMU.
USIKU.
HATA KAMA NINGELIJUA PA KUWATAFUTA JAMAA WANGU SIDHANI NINGELIWAPATA HIVI KARIBUNI.
TUTAFUTE TU MAHALI PA KUKAA SIKU CHACHE ZIJAZO.
TUTAWATAFUTA BAADAYE. NAHITAJI -- AH! NILALE.
HIVI SIVYO NILIVYOTARAJIA.
UKO SAWA?
MGONGO WANGU KIDOGO...HAUKO SAWA. TUTAFUTE NYUMBA YA WAGENI...
TAFADHALI BWANA, KUNA CHUMBA?
INAKAA KAMA NINA CHUMBA? NILIKODISHA VYOTE VIWILI WIKI ILIYOPITA!
TULITUMAINI UNA CHUMBA KIDOGO.
TWAWEZA KUKAA PAMOJA.
POLE MAANAKE FAMILIA ILIYO KODISHA CHUMBA CHA JUU HAWAPENDELEI KUTUMIA PAMOJA NANYI, TAYARI MIE NIKO PAMOJA NA FAMILIA NYENGINE CHUMBA CHA CHINI!
HODI! NJOO TAFADHALI!
TWENDE YOSEFU, HAWATATUFUNGULIA MLANGO.
KUTOKANA NA KELELE ZILIZO HUMO NDANI NYUMBA ISHAJAA.
TAFADHALI BWANA, HAKUNA ALIYE NA CHUMBA CHA KUTUPATIA.
POLE!
TWAHITAJI MAKAO. WAONA MKE WANGU --
NDIO! ITABIDI MPATE MAHALI HIVI KARIBUNI; YUKO TAYARI KUPASUKA!


LUKA 2:6-7


BWANA, TAFADHALI, MIMI NA MKE WANGU TWAHITAJI MAHALI PA KUKAA.
HATUHITAJI MAHALI PAKUBWA, PA KUJIKINGA NA BARIDI TU.
MUNGEKUJA MAPEMA.
NDIO.
SINA VYUMBA VYA KUWAPA.
LAKINI NAWEZA KUWA NINA MAHALI PENGINE.
KAMA HAMNA WASIWASI NAWEZA KUWAPATIA MAKAO KWA SIKU CHACHE.
SI CHUMBA KIZURI KOTE BETLEHEMU.
LAKINI HAKIVUJI NA NI BEI NAFUU.
ASANTE BWANA.
LALA HAPA.
JARIBU KULALA VIZURI.
YOSEFU TUTAHITAJI MKUNGA.
KWELI.
KWA SIKU CHACHE TUTAKUWA TUMEWAPATA JAMAA ZANGU. NINA UHAKIKA WATAJUA MKUNGA.
YOSEFU MIMI NA WEWE HATUWEZI KUZALISHA MTOTO HUYU PEKE YETU!
SAWA, NITAMUULIZA MWENYE NYUMBA YA WAGENI KESHO --
SASA!
LUKA 2:6-7


AH!
LAKINI SIFAI KUKUACHA PEKE YAKO!
KUNA WAKATI YOSEFU.
INAANZA TU, NADHANI.
ENDA! LAKINI HARAKISHA!
NTAONA KAMA MWENYE NYUMBA YA WAGENI ANAJUA YEYOTE!
NARUDI SASA HIVI!
HODI
MKE WANGU!
ANAJIFUNGUA!
NINI KINAENDELEA?
MTOTO YWAJA! TWAHITAJI MKUNGA!
RUDI ALIKO MKEO!
NTATAFUTA!
WATAKUA HAPA WAKATI WOWOTE.
KILA KITU KITAKUWA SAWA.
NAJUA.
LUKA 2:6



NIMEPATA MTU.
WEWE NDIYE BABA?
MIMI NI MUMEWE.
NYINYI WANAUME HAMFAI KUWA HAPA.
UWAANGALIE VIZURI!
HUYO NI MTOTO WA KIPEKEE!
NDIO, NDIO, TWAJUA.
LAZIMA MUENDE SASA.
SASA MSICHANA, NIAMBIE UNAVYOHISI.
NI SAWA UNAFANYA VIZURI.
IMEZIDI! SIWEZI!
HIVI NDIVYO NINGEPENDA UFANYE UKIHISI UCHUNGU TENA...
LUKA 2:7


BWANA!
UMEPATA MVULANA!
NI MREMBO.
NDIO. NI MREMBO.


MALISHONI HAPO KARIBU WACHUNGAJI WALIWACHUNGA KONDOO WAO.
BABU, KWELI NI LAZIMA SOTE TUWE HAPA NJE?
KUNA BARIDI NA NIMECHOKA!
AH, TOBIN! KIVIPI HUWEZI KUPENDELEA KUWA NJE USIKU KAMA HUU WA LEO?
TUNAWALINDA VIUMBE WENYE THAMANI YA JUU!
KONDOO HAWA WANATUPA SUFI YA KUWAKINGA WATU WETU DHIDI YA BARIDI; NYAMA NA JIBINI YA KULISHA WATU WETU; MAZIWA YA KUKATA KIU CHA WATU WETU!
MFALME DAUDI MWENYEWE ALIKUA MCHUNGAJI -- LABDA MIFUGO YETU INA ASILI YA MOJAWAPO WA KONDOO WAKE!
NA WATOTO WATAOZALIWA NA WAKE HAWA WAWEZA KUTUMIKA KAMA DHABIHU KWA DHAMBI ZA --
NINI KINAENDELEA?
BABU, ANGALIA!
USIOGOPE.
LEO, KWENYE MJI WA BETLEHEMU, JIJI LA DAUDI, MKOMBOZI WENU AMEZALIWA!
NI KRISTO BWANA WENU!
MTAMPATA AMEFINIKWA NGUO NA AMELALA NDANI YA HORI!


UTUKUFU KWA MUNGU ALIYE JUU! DUNIANI AMANI KWA WATU WOTE ALIOPENDEZWA NAO!


SAMAHANI...
TULIAMBIWA... YAANI, TUMEARIFIWA --
MALAIKA WALITUAMBIA MTOTO MASSIAH AMEZALIWA!
MALAIKA?
MALAIKA. UNASHANGAA?
WALISEMA MTOTO ATAKUWA HORINI NA HILI NDIO HORI TULILOPATA LENYE MTOTO NDANI!
TUMEANGALIA ZOTE!
NDIYE HUYU?
NDIO.
JINA LAKE NI NANI?
YESU.
YAMAANISHA...


...BWANA NI MKOMBOZI.

"THE BIBLE EXPLAINED
IN EVERY LANGUAGE."





SUPERBIBLE.TV